BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA

MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU

KIDATO CHA NNE

021

KISWAHILI

(Kwa Watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)

MUDA: Saa 3 **Jumatatu, 24 Agosti 2026 Mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **kumi na sita (16),** sehemu B ina alama **Hamsini na nne (54)** na sehemu C ina alama **thelathini (30).**
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

ShuleLibrary.com

SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.

(i) Mada ya uandishi huambatana na taratibu zake ikiwemo matumizi ya herufi kubwa. Ipi kati ya sentensi zifuatazo haielezi matumizi yake?

A. Hutumika katika majina ya watu
B. Hutumika katika majina ya jamii
C. Hutumika kila mwanzo wa sentensi
D. Hutumika baada ya alama ya nukta
E. Hutumika katika maneno ya vifupisho

(ii) Mzee Masumbuko alipokuwa akiwasimulia hadithi wajukuu wake kuhusu ugomvi wa simba na chui, alisikika akisema "chui **alichungulia kaburi**" kutokana na kipigo alichokipata kutoka kwa simba. Unafikiri kauli iliyopigiwa mstari ina maana gani?

A. Alikaribia kifo
B. Alikiona kifo
C. Alitabiri kifo
D. Aliota kifo
E. Alikimbia kifo

(iii) Jamali na Jamili ni ndugu waliokuwa wanabishana kuhusu muundo wa sentensi isemayo, "Wao wataondoka na sisi tutapika chakula". Upi ni muundo sahihi wa sentensi hiyo?

A. W T U W T E
B. E T U W T N
C. N T U W T N
D. V T U W T E
E. W T U W T N

(iv) Wanafunzi wa shule ya sekondari Mabondeni walipewa kazi ya kubainisha aina ya usomaji unaosaidia kupima uwezo wa kutamka maneno kwa ufasaha na kutumia lafudhi ya lugha husika. Je, ipi ni aina sahihi kati ya zifuatazo?

A. Kusoma kwa burudani
B. Kusoma kwa ukimya
C. Kusoma kwa sauti
D. Kusoma kwa makini
E. Kusoma kwa ziada

(v) Mzee Sadiki alimtaka binti yake wa kidato cha nne amuandalie tangazo la biashara yake ya simu za mkononi. Jambo lipi kati ya haya yafuatayo atalizingatia?

A. Aina ya bidhaa na idadi ya wateja
B. Aina ya bidhaa na bei ya kila moja
C. Aina ya kichwa cha tangazo la bidhaa
D. Kichwa cha tangazo na lengo lake
E. Kichwa cha tangazo na bei ya kila bidhaa

Shulelibrary.com

(vi) Kama mbobezi wa lugha ya Kiswahili na mwanafasihi Hodari, onesha namna gani unaweza kuwashawishi watu waliokuzunguka kuwa "Ngonjera ni sawa na maigizo." Kupitia hoja zifuatazo:

A. Ngonjera huwa ina kibwagizo
B. Ngonjera huwa inatumia lugha ya kinathari
C. Ngonjera huwa ina urari wa vina na mizani
D. Ngonjera huwa na wahusika watendaji
E. Ngonjera huwa inamilikiwa na jamii

(vii) Ufupishaji wa habari kwa mdomo una misingi na miiko yake inayopaswa kuzingatiwa. Upi kati ya ifuatayo ni mojawapo ya msingi wake?

A. Mtiririko wa mazungumzo
B. Kuzungumza kwa sauti
C. Kuwa makini kwa kinachosemwa
D. Alama za uandishi
E. Wazo kuu

(viii) Kiimbo huonesha lengo la mzungumzaji wa lugha husika. Je, sentensi isemayo "Soma kwa bidii", huonesha dhima ipi kati ya zifuatazo?

A. Kuuliza swali
B. Kutoa amri
C. Kutoa taarifa
D. Kuonesha hisia
E. Kusisitiza jambo

(ix) "Papai limeiva nyumbani lakini nashindwa kulila."Kauli hii inawakilisha kipera gani cha semi?

A. Mizungu
B. Methali
C. Nahau
D. Misemo
E. Kitendawili

(x) Wanakijiji wa kijiji cha Bukole walitaka kueleza mahitaji yao mbele ya kiongozi wao kwa njia ya maandishi. Je, watatumia andiko gani kati ya haya yafuatayo?

A. Hotuba
B. Kumbukumbu za mkutano
C. Risala
D. Insha ya kiada
E. Barua

Shulelibrary.com

2. Oanisha asasi za kukuza na kueneza Kiswahili kutoka katika **Orodha A** na mwaka wake wa kuanzishwa kutoka **Orodha B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.

ORODHA A	ORODHA B
(i) TUKI	A. 2009
(ii) BAKIZA	B. 2012
(iii) TATAKI	C. 1979
(iv) BAKITA	D. 2003
(v) TAKILUKI	E. 1970
(vi) SKILUKI	F. 1972
	G. 1974
	H. 1967

SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

3. "Mtindo wa lugha hutofautiana kutokana na muktadha na shughuli iliyopo."
   (a) Istilahi ipi hutumika kuwakilisha dhana hiyo?
   (b) Eleza dhima tano (5) za istilahi uliyoitaja katika kipengele (a) hapo juu.

4. Katika mjengo wa tungo za Kiswahili, kirai nomino hujitokeza katika mazingira mbalimbali. Bainisha mazingira hayo kwa hoja sita (6) na toa mfano mmoja kwa kila hoja.

5. Maneno ya Kiswahili hayapo kiholelaholela, bali huundwa kwa kuzingatia njia maalumu ikiwemo njia ya ufupishaji.
   (a) Eleza maana ya njia hiyo.
   (b) Fafanua aina kuu tatu (3) za njia hiyo.

6. Kiswahili kimekua kutokana na shughuli mbalimbali kabla na baada ya uhuru. Kwa maarifa uliyoyapata darasani, eleza kwa kina mchango wa dini na vyombo vya habari katika ukuaji huo. Toa hoja tatu (3) kwa kila upande.

7. Fikiria kwamba unapaswa kuandika barua kwa wazazi wako ili kuomba vifaa vya mtihani. Je, mambo yapi utayazingatia katika muundo wa barua yako? (Toa hoja sita (6) za mwanzo).

8. Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali ya hapo chini.
   Kijiji cha Maringo hujulikana sana katika kata ya Kambakwale. Kijiji hicho kilikuwa kinadumisha mila na desturi za kipekee, ukilinganisha na vijiji vingine. Watu wake hawakuchangamana na jamii yoyote katika kata hiyo, waliishi kwa kufuga na kula nyama.

   Wakazi wa Kijiji hicho walikuwa wakarimu sana kwa wageni. Waliweza kumkarimu kila mtu hata mtu wasiyemjua, wakiamini kuwa "mgeni aje mwenyeji apone". Methali hiyo kwa wakazi wa Kijiji hicho ilikuwa na maana kubwa sana, kama wasemavyo wahenga kuwa "Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti". Kila aliyepita kijijini hapo, ulikuwa mwisho wa maisha yake.

Shulelibrary.com

Maswali:

(a) Bainisha kipengele cha matumizi ya lugha kilichotumika.

(b) Wanakijiji wa Maringo walijishughulisha na kazi ipi ya uzalishaji mali?

(c) Toa maana za methali mbili zilizotumika katika habari hiyo.

(d) Jambo gani lilikipa umaarufu Kijiji cha Maringo?

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **tisa (9) ni la lazima.**

ORODHA YA VITABU

Ushairi:

Wasakatonge	-	M.S. Khatibu (DUP)
Malenga Wapya	-	TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya Chekacheka	-	T.A. MVUNGI (EP&D LTD)

Riwaya:

Takadini	-	Ben J. Hamson (MBS)
Watoto wa Mama N'tilie	-	E. Mbogo (HP)
Joka la Mdimu	-	J. Safari (HP)

Tamthiliya:

Orodha	-	Steve Reynolds (MA)
Ngoswe- Penzi Kitovu cha Uzembe	-	E. Semzaba (ESC)
Kilio Chetu	-	Medical Aid Foundation (TPH)

Shulelibrary.com

9. Kauli za washairi ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii bora. Thibitisha usemi huu kwa hoja tatu kutoka katika kila diwani kwa kutumia diwani mbili ulizosoma.

10. Katika kuleta upekee na kupamba kazi zao, watunzi wa kazi za fasihi wamekuwa wakitumia mitindo tofauti tofauti. Kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma, thibitisha dai hilo kwa hoja tatu kwa kila kitabu.

11. Mandhari katika fasihi ni kipengele muhimu katika kuibua hisia na mambo mbalimbali. Kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma, onesha ukweli wa kauli hii.

Wabillah Tawfiiq